

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Barua pepe : [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

*Katavi*  
13 Julai, 2024

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewapongeza wakulima kote nchini kwa kiwango cha uzalishaji wa chakula na kuifanya nchi kuwa na utoshelevu wa chakula unaozidi asilimia 120.

Rais Dkt. Samia ametoa pongezi hizo leo wakati akihutubia katika kilele cha Wiki ya Wazazi pamoja na mkutano wa hadhara iliyofanyika katika viwanja vya Azimio, Mpanda mjini.

Aidha, Rais Dkt. Samia amesema utoshelevu huu umesaidia nchi kudhibiti mfumuko wa bei ambao umebaki asilimia 3 na hivyo kuwaepusha wananchi na ugumu wa maisha unaotokana na uhaba wa chakula na mfumuko wa bei.

Rais Dkt. Samia amezitaka Halmashauri zote katika mkoa wa Katavi kuacha tabia ya kuwatoza wananchi ushuru wa mazao kwa kiasi kisichozidi tani moja na kufuata maelekezo yaliyotolewa na Serikali hapo awali.

Kwa upande mwingine, Rais Dkt. Samia amesema Serikali ipo mbioni kukamilisha miradi ya umeme itakayoiunganisha Mikoa ya Katavi na Kigoma kwenye Gridi ya Taifa ifikapo Oktoba 2024 na hivyo kuwa na umeme wa uhakika.

Awali asubuhi, Rais Dkt. Samia alikagua mradi wa kupokea, kupoza na kusambaza umeme wa Inyonga ambao ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa vituo vitatu vya Ipole (Sikonge), Inyonga (Mlele) na Mpanda wenye thamani ya shilingi bilioni 48.

Mradi huu unaenda sambamba na mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Tabora hadi Katavi wenye thamani ya shilingi bilioni 116.29 unaotarajia kukamilika ifikapo mwezi Oktoba mwaka huu.

Rais Dkt. Samia pia amesema Serikali inaendelea kuifungua Katavi kiuchumi kupitia miundombinu ya usafirishaji ikiwemo ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Mpanda na Bandari ya Karema ambayo italeta fursa za kibiashara na ajira kwa wananchi.

A blue ink signature of Sharifa B. Nyanga.

Sharifa B. Nyanga  
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

